# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

***(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)***

**Sehemu ya CXXIX Nam. 6871** **30 Oktoba, 2020** **Bei Shs. 3000/=**

*Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti* *Hutolewa kila Ijumaa*

**YALIYOMO** Ukurasa

Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Nam. 7 ya mwaka 2014.
Kanuni za Huduma zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
[Chini ya kifungu cha 94]

**SEHEMU YA SHERIA**

Tangazo la Sheria lililotajwa hapo chini limetangazwa katika Gazeti Rasmi hili.

**Matangazo ya Sheria**

Nam. 159:- Kanuni za Huduma zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa



Scanned with CamScanner

**TANGAZO NAM: 96**

## SHERIA YA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MTAA NAM. 7 YA MWAKA 2014

---

## KANUNI ZA HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA.

**(Chini ya Kifungu cha 94)**

---

**KWA UWEZO** niliopewa chini ya kifungu cha 94 cha Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Nam.7 ya mwaka 2014, Mimi HAJI OMAR KHERI Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, nafanya marekebisho ya Kanuni Kanuni Za Huduma Zinazotolewa Na Mamlaka Za Serikali Za Mitaa, 2017 kama ifuatavyo:

### SEHEMU YA KWANZA
### UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Huduma zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Marekebisho), 2020 na zitaanza kutumika baada ya kusainiwa na Waziri na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

2. Kanuni hizi zitasomeka pamoja na Kanuni Za Huduma Zinazotolewa Na Mamlaka Za Serikali Za Mitaa, 2017 katika sehemu itajulikana "Kanuni Mama"

### SEHEMU YA PILI
### MAREKEBISHO YA VIFUNGU

Marekebisho ya Kanuni ya 6

3. Kanuni Mama inarekebishwa katika Kanuni ya 6

(a) kuweka Kanuni 6 ya awali kuwa 6(1)
(b) kuongeza kanuni ndogo ya (2) baada ya kanuni ya 6(1) kama ifuatavyo;

"6(2) Bila ya kuathiri Kanuni Ndogo ya (1) ya Kanuni hii mtu yeyote anaefanya shughuli za kiuchumi na anayewajibika kulipa Ada ya usafi kwa mwaka, atalipa Ada hiyo ya usafi wakati wa kukata leseni"

Marekebisho ya Kanuni ya 31.

**4.** Kanuni Mama inarekebishwa katika Kanuni ya 31 kwa kufuta maneno "Sheria ya Leseni za Biashara Namba 13 ya 2014" na kuweka maneno "Sheria ya Usimamizi wa Leseni za Biashara namba 13 ya 2013".

Scanned with CamScanner

**5.** Kanuni Mama inarekebishwa katika Kanuni ya 34 kwa kufuta Kanuni Ndogo ya (1) ya Kanuni ya 34 na kuweka Kanuni mpya ya 34(1) kama ifuatavyo; Marekebisho ya Kanuni ya 34.

"34(1) Mtu yeyote anaefanya Biashara Ndogo Ndogo zilizoainishwa katika Jadweli la Tano la Kanuni hizi, ndani ya eneo la Serikali ya Mtaa atalazimika kulipia Ada ya Usajili na kupatiwa kitambulisho maalum, kutokana na eneo analofanyia biashara"

**6.** Kanuni Mama inarekebishwa katika Kanuni ya 48 kwa kufuta Kanuni ya 48 na kuweka Kanuni mpya ya 48 kama ifuatavyo; Marekebisho ya Kanuni ya 48.

"48 Mtu yeyote anayenadisha bidhaa katika eneo la Mamlaka atalazimika kulipia Ada ya Beji ya Udalali wa minada kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Nne. Ada ya Beji ya Udalali wa minada.

**7.** Kanuni Mama inarekebishwa katika Kanuni ya 50 kwa kufuta Kanuni ya 50 na kuweka Kanuni mpya ya 50 kama ifuatavyo; Marekebi-sho ya Kanuni ya 50.

"50. Mtu yeyote anaetoa huduma za Usafiri wa dala dala na gari za shamba katika eneo la Serikali ya Mtaa atawajibika kulipia Ada ya Usafi kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Nne, wakati wa kulipia Ada ya ruhusa ya njia kwa taasisi inayohusika na masuala ya usafiri wa barabarani" Ada ya Usafi kwa Gari za Abiria.

**8.** Kanuni Mama inarekebishwa kwa kufuta Kanuni ya 51 Kufuta Kanuni ya 51.

**9.** Kanuni Mama inarekebishwa katika Kanuni ya 59 kwa kufuta Kanuni ya 59(1) na kuweka Kanuni mpya ya 59(1) kama ifuatavyo; Marekebi-sho ya Kanuni ya 59.

"59. (1) Mtu yeyote anayefanya biashara ya kuuza dagaa au mwani katika Masoko yaliyo nje ya Zanzibar atalazimika kulipa Ada ya Usafirishaji wa Dagaa au Mwani kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Pili. Ada ya Usafirishaji wa Dagaa au Mwani

**10.** Kanuni Mama inarekebishwa kwa kufuta Kanuni ya 60. Kufuta Kanuni ya 60.

**11.** Kanuni Mama inarekebishwa kwa kufuta Kanuni ya 61 Kufuta Kanuni ya 61.

**12.** Kanuni Mama inarekebishwa kwa kufuta Kanuni ya 64 Kufuta Kanuni ya 64.

**13.** Kanuni Mama inarekebishwa kwa kufuta Kanuni ya 66 Kufuta Kanuni ya 66.

**14.** Kanuni Mama inarekebishwa kwa kufuta Jadweli la Kwanza na kuweka Jadweli jipya la Kwanza, kama ifuatavyo; Marekebi-sho ya Jadweli la Kwanza.

Ada ya Fomu na Leseni

Scanned with CamScanner

Marekebisho ya Jadweli la Pili.

**15.** Kanuni Mama inarekebishwa kwa kufuta Jadweli la Pili na kuweka Jadweli jipya la Pili, kama ifuatavyo;

Ada ya Usafirishaji wa Mazao ya Misitu, Maliasili, Dagaa na Mwani

Kuongeza Jadweli jipya la Nne.

**16.** Kanuni Mama inarekebishwa kwa kuongeza Jadweli jipya la Nne mara baada ya Jadweli la Tatu kama ifuatavyo;

Ada ya Usafi, Ujenzi na Huduma Nyenginezo.

Kuongeza Jadweli jipya la Tano.

**18.** Kanuni Mama inarekebishwa kwa kuongeza Jadweli jipya la Tano mara baada ya Jadweli la Nne kama ifuatavyo;

Ada ya Usajili kwa Biashara Ndogo

Ndogo.

Kuongeza Jadweli jipya la Sita.

**19.** Kanuni Mama inarekebishwa kwa kuongeza Jadweli jipya la Sita mara baada ya Jadweli la Tano kama ifuatavyo;

Fomu ya maombi ya Leseni ya Biashara.

Kuongeza Jadweli jipya la Saba.

**20.** Kanuni Mama inarekebishwa kwa kuongeza Jadweli jipya la Saba mara baada ya Jadweli la Sita kama ifuatavyo;

Fomu ya Usajili wa Vyombo vya Uvuvi, Mabango, Matangazo na Minara

**IMETIWA** Saini na Waziri tarehe 22 Oktoba, 2020.

(HAJI OMAR KHERI)
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ ZANZIBAR**

Scanned with CamScanner

# MAJEDWALI

## JADWELI LA KWANZA

## (Ada ya Fomu na Leseni)

**(Imeundwa chini ya Kanuni 31(2) na 32)**

| HUDUMA | CHANZO CHA MAPATO | KIWANGO (TZS) |
|---|---|---|
| FOMU | Maombi ya Leseni ya biashara | 10,000/- |
| | Maombi ya leseni ya Vileo | 150, 000/- |
| | Maombi ya leseni nyumba za kulala wageni | 100,000/- |
| | | |
| LESENI | **AINA YA BIASHARA** | **KWA MWAKA** |
| | **VILEO:** | |
| | Hoteli yenye nyota 5 na 4 | 5,000,000/- |
| | Hoteli yenye nyota 3 na 2 | 4,000,000/- |
| | Hoteli yenye nyota 1 | 3,000,000/- |
| | Hoteli yenye nyota A, AA, AAA na chini ya kiwango | 2,000,000/- |
| | Bar | 2,000,000/- |
| | Maduka/store | 2,000,000/- |
| | **MADUKA NA VIWANDA** | |
| | **MTAJI** | **Ada ya Leseni** |
| | Isiyozidi 1,000,000 | 40,000 |
| | Inayozidi 1,000,000 - 5,000,000 | 80,000 |
| | Inayozidi 5,000,000 - 10,000,000 | 100,000 |
| | Inayozidi 10,000,000 – 20,000,000 | 150,000 |
| | Inayozidi 20,000,000– 40,000,000 | 200,000 |
| | Inayozidi 40,000,000- 60,000,000 | 250,000 |
| | Inayozidi 60,000,000 – 80,000,000 | 300,000 |
| | Inayozidi 80,000,000 – 100,000,000 | 350,000 |
| | Inayozidi 100,000,000 –150,000,000 | 400,000 |
| | Inayozidi 150,000,000 – 200,000,000 | 450,000 |
| | Inayozidi 200,000,000 – 250,000,000 | 500,000 |
| | Inayozidi 250,000,000 – 300,000,000 | 550,000 |
| | Inayozidi 300,000,000 | 600,000 |
| | **BIASHARA NYENGINEZO** | |
| | Yadi za magari | 400, 000/- |
| | Fundi Ushoni vyarahani zaidi ya 3 | 60,000/- |
| | Huduma za Simu (Mawakala) | 200,000/- |
| | Mikahawa Mikubwa | 300,000/- |
| | Mikahawa Midogo | 50,000 /- |
| | Mikahawa ya kati | 150,000/- |
| | Huduma za Ofisi ndogo | 150,000/- |
| | Huduma za Ofisi kubwa | 300,000/- |
| | Ghala dogo | 300,000/- |
| | Ghala kubwa | 500,000/- |
| | Huduma za Mitandao (Internet Café) | 200,000/- |
| | Gereji ndogo | 150,000/- |
| | Gereji kubwa | 400,000/- |
| | Kuosha Vyombo vya Moto (Car Wash) | 200,000/- |
| | Kitalu binafsi | 80,000/- |
| | Kampuni zinazotoa huduma | 300,000 |
| | Vitu chakavu (Makachara) wadogo | 100,000/- |
| | Vitu chakavu (Makachara) wakubwa | 200,000/- |
| | Kumbi za shughuli (Hall) | 200,000 /- |
| | Benki | 1,000,000/- |
| | Mashirika | 1,000,000/- |
| | Bureau de change | 500,000/- |
| | Wakala wa Benki | 200,000/- |
| | Bekari | 150,000/- |
| | Wakala wa usafirishaji na uagiziaji | 300,000/- |
| | Dobi (laundry services) wadogo | 150,000/- |
| | Dobi (laundry services) wakubwa | 250,000/- |
| | Saluni ndogo | 80,000/- |

Scanned with CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| | Skuli binafsi za Maandalizi (Nursery) | 100,000/- |
| | Skuli binafsi za Maandalizi na Msingi | 250,000/- |
| | Skuli za binafsi Maandalizi, Msingi na Sekondari (Secondary) | 500,000/- |
| | Dispensary | 200,000/- |
| | Hospitali binafsi | 400,000/- |
| | Nyumba za kulala Wageni | 30,000/- kwa chumba kwa mwaka, leseni kwa mwaka isipungue 150,000/- |
| | Waziba Mipira. | 80,000/- |
| | Wanauza na kuziba mipira | 150,000/- |
| | Sheli ndogo ya Mafuta ya taa | 120,000/- |
| | Sheli zinazoambatana na maduka | 1,600,000/- |
| | Sheli zisizoambatana na maduka | 1,000,000/- |
| | Vyombo vya Usafiri vya kuchukulia watalii kwa matemebezi wa visiwani na mafunguni | 100,000/- kwa mwaka |

## JADWELI LA PILI

**(Ada ya Usafirishaji wa Mazao ya Misitu, Maliasili, Dagaa na Mwani)**

**(Imeundwa chini ya Kanuni 57, 58 na 59)**

| MAZAO | AINA YA MAZAO | KIWANGO (TZS) |
|---|---|---|
| **MISITU NA MALIASILI** | Kuni | 500/- kwa mzigo |
| | Makaa | 500 /- polo au gunia |
| | Nguzo au miti | 2000/- kwa korija |
| | Fito | 500 /- kwa mzigo |
| | Asali | 2000/- debe au galoni |
| | Nta | 500/- kwa kilo |
| | Mbao | 500/- kwa ubao |
| | Maliasili zisizorejesheka | 1500/- kwa tani moja |
| **DAGAA NA MWANI** | Dagaa, Unga wa dagaa | 1000/- kwa tani moja |
| | Mwani | 5000/- kwa tani moja |

Scanned with CamScanner

## JADWELI LA NNE

**(Ada ya Usafi, Ujenzi na Huduma Nyenginezo)**

**(Imeundwa chini ya Kanuni 6, 50, 54, 62 na 77(2))**

| MAENEO | AINA YA BIASHARA | KIWANGO (TZS) |
|---|---|---|
| USAFI | Vituo vya Mafuta | 600,000 kwa mwaka |
| | Viwanda vikubwa vilivyosajiliwa na ZIPA | 600,000 kwa mwaka |
| | Viwanda vidogo | 240,000 kwa mwaka |
| | Maduka na Ofisi | 50,000 kwa mwaka |
| | Gereji | 50,000 kwa mwaka |
| | Nyumba za kuishi | 3000 kwa mwezi |
| | Hoteli kubwa | 1,250,000 kwa mwezi |
| | Hoteli Ndogo | 500,000 kwa mwezi |
| | Nyumba za kulala wageni | 100,000 kwa mwezi |
| | Kuzibua Michirizi ya kawaida | 150,000 kwa uzibuaji |
| | Huduma za kusafisha choo, makaro | 150,000 kwa trip |
| | Kuunganisha mitaro | 50,000 kwa mwaka |
| | Ghala | 100,000 kwa mwaka |
| | Mikahawa | 50,000 kwa mwaka |
| | Yadi ya magari | 100,000 kwa mwaka |
| | Gari za abiria (Daladala na Gari za Shamba) | 50,000 kwa mwaka |
| NYENGINEZO | Maegesho ya magari | 1000/- kwa saa |
| | Maegesho ya Vespa,Pikipiki na Honda | 500/- kwa saa |
| | Uingizaji wa mnyama ndani ya eneo la Mamlaka ya Serikali za mitaa | 10,000 Kwa mnyama. |
| | Machinjio | 5000 kwa mnyama |
| | Beji ya udalali | 100,000/- kwa mwaka |
| | Minara | 2 ,500,000 kwa mwaka |
| | Maonyesho / Matamasha | 5000 kwa siku |
| UJENZI | Ada ya fomu ya Kibali cha Ujenzi | 20,000/- kwa ombi |
| | Nyumba ya Kuishi | 50,000 – 150,000 |
| | Nyumba za Kulala Wageni | 200,000- 350,000 |
| | Nyumba za Ghorofa | 1,000,000 – Kwa Ghorofa |
| | Ukuta (Fensi) | 6,500 kwa mita |
| | Minara ya Simu | 5% ya gharama ya ujenzi |
| | Vituo vya mafuta | 500,000 – 1,000,000 |
| | Mabwawa (Swimming Pool) | 1,000,000 |
| | Shule | 500,000 – 1,500,000 |
| | Zahanati | 500,000 – 1,500,000 |
| | Mlango wa Biashara | 50,000– 100,000 |
| | Ghala | 500,000 – 1,000,000 |
| | | |

## JADWELI LA TANO

**(Ada ya Usajili kwa Biashara Ndogo Ndogo)**

**(Imeundwa chini ya kanuni ya 34)**

| MAENEO | AINA YA BIASHARA | KIWANGO (TZS) |
|---|---|---|
| Wafanyabiashara katika Maeneo Yaliyoruhusiwa | Vitafunwa, Mbogamboga, Matunda, Vyakula, Samaki, Vinywaji, Mazao ya Misitu, Mafundi, Wauza Mikate, Wauza/Waanika Dagaa na biashara zinazofanana na hizo | 30,000 kwa mwaka |
| | | |
| Wafanyabiashara katika Maeneo Maalum | Vitafunwa, Mbogamboga, Matunda, Vyakula, Samaki, Vinywaji na biashara na huduma nyenginezo katika maeneo hayo maalum | 100,000/- kwa mwaka |

Scanned with CamScanner

**JADWELI LA SITA**

**(Fomu ya Maombi ya Leseni ya Biashara)**

**(Imeundwa chini ya kanuni ya 31(2))**

***LGA***

***200*** **MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA**

**(NEMBO YA MAMLAKA HUSIKA)**

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA NAMBA 7 YA 2014**

**FOMU YA MAOMBI YA LESENI YA BIASHARA**

| Picha |
|---|
| |

**Nambari ya Usajili ya Muombaji**

..................................................

**1. TAARIFA BINAFSI** *(kama ni kampuni andika taarifa za mmiliki na jina la kampuni)*

| Jina la Kwanza | | Jina la Pili | | Jina la Tatu | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |
| Anuani(SLP) | | | ***Weka alama ya (√ )*** | Mme | | Mke |
| | | Uraia | | Aina ya kitambulisho | | |
| | | | | | | |
| Nambari ya simu | | Nambari ya Kitambulisho | | | | |
| | | | | | | |
| Anuani ya Makaazi *(nambari ya nyumba)* | | | | | | |
| Mkoa | Wilaya | Shehia | | Mtaa | | |
| | | | | | | |

**2. TAARIFA ZA BIASHARA** *(Sehemu hii ijazwe na muombaji wa leseni)*

| Jina la Kampuni/ Ubia/Binafsi | | Jina la Biashara | | Aina ya biashara |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| Jumla | Rejareja | Eneo la biashara | | |
| | | Wadi | | |
| Nyumba yangu | Nimekodi | Shehia | | |
| | | Mtaa | | |
| Mtaji wa biashara | | Makisio ya mauzo kwa mwaka | | |
| Nambari ya leseni iliyopita *(kama ni ombi jipya andika **JIPYA**)* | | Malipo iliyotozwa | | Tarehe iliyotolewa |
| | | | | |

**3. MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA** *(weka alama ya √ mbele ya "Ndiyo" au "Hapana")*

| Kiongozi wa Serikali ya Mtaa | Jina la Shehia / Wadi | Anatoa huduma katika eneo lako? | | | | Mhuri, tarehe na saini |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Sheha | | Ndiyo | | Hapana | | |
| Diwani | | Ndiyo | | Hapana | | |

**4. TAMKO**

Mimi ______________________________ nathibitisha kwamba yote niliyoeleza hapo juu ni kweli kama nijuavyo, na kwamba nimekubaliana na masharti na taratibu zote za leseni kama zilivyo ainishwa katika fomu hii.

Tarehe _____________ Cheo _______________ Sahihi ya muombaji _____________

***5.*** **KWA MATUMIZI YA OFISI TU**

| ***Maoni kuhusiana na ombi lililoletwa*** | | | |
|---|---|---|---|
| Afisa/Mkaguzi | Apewe/Asipewe | Tarehe | Muhuri na saini ya Afisa |
| Afisa wa kitengo cha Divisheni | | | |
| Afya na Mazingira | | | |

| ***Maoni ya Afisa Tathmini/Kitengo husika*** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kiwango anachostahiki kulipa | Faini | Jumla | Tarehe | Saini |
| | | | | |
| Imethibitishwa na Mkuu wa Idara ya Mipango, Utawala na Rasilimali Watu | | | | |

Scanned with CamScanner

**6. MASHARTI YA MAOMBI NA UTHIBITISHO WA MUOMBAJI**

i) Mteja au mfanyabiashara anatakiwa kufika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kufanya maombi ya Leseni.

ii) Muda wa hiari uliopangwa kukata leseni ya biashara kisheria ni kuanzia Januari hadi Machi. Na mara tu baada ya muda wa hiari kumalizika utalazimika kukata leseni pamoja adhabu ya faini ya 20% ya bei halisi ya leseni unayoomba.

iii) Hakikisha kuwa unalipa ada ya usafi wa mazingira kwa wakati unaostahiki (kwa mwaka).

iv) Hakikisha Fomu yako inaambatanishwa na vielelezo vinavyohusika kwa biashara zinazohusu ruhusa au uthibitisho wa Taasisi nyengine, biashara hizo ni kama maduka ya nyama, maduka ya dawa baridi, maduka ya Gesi, Kampuni, Vituo vya Afya, Skuli n.k. isipokuwa kwa vinavyomilikiwa na Serikali.

## JADWELI LA SABA

### (Fomu ya Usajili wa Vyombo vya Uvuvi, Mabango, Matangazo na Minara)

**(Imeundwa chini ya Kanuni 46, 47 na 63)**

**MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA** **LGA201**

**(NEMBO YA MAMLAKA HUSIKA)**

Picha

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA NAMBA 7 YA 2014**

**FOMU YA USAJILI**

**Nambari ya Usajili ya Muombaji**

..............................................

**1. TAARIFA BINAFSI** *(kama ni kampuni andika taarifa za mmiliki na jina la kampuni)*

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Jina la Kwanza | Jina la Pili | | Jina la Tatu | | | |
| | | | | | | |
| Anuani(SLP) | | ***Weka alama ya (√ )*** | Mme | | Mke | |
| | Uraia | | Aina ya kitambulisho | | | |
| | | | | | | |
| Nambari ya simu | | Nambari ya Kitambulisho | | | | |
| | | | | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Anuani ya Makaazi *(nambari ya nyumba)* | | | |
| Mkoa | Wilaya | Shehia | Mtaa |
| | | | |

**2. TAARIFA ZA HUDUMA ZA UVUVI** *(weka alama ya √ kwenye huduma unayoomba)*

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ***(Sehemu hii ijazwe na muombaji wa leseni ya Uvuvi)*** | | | | | | | | |
| Leseni ya | Chombo cha uvuvi | | Aina ya chombo | Faiba | Ngwanda | Dau | Ngalawa | Taja jina la Diko |
| | Mvuvi/Bahariá | | | | | | | |
| Wadi | | | | Shehia | | | | |

Scanned with CamScanner

**3. MABANGO, MATANGAZO NA MINARA YA MAWASILIANO** *(weka alama ya √ panapohusika)*

| *Kama ni Mabango jaza hapa* | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Aina ya bango | La kielektroniki | Lisilo la kielektroniki | Posters | Gazebo | Banner | Roadshow | Nyegine *(itaje)* | | |
| | | | | | | | | | |
| Vipimo vya bango | | Urefu | | Upana | | (futi) | | (mita) | |
| Eneo linapoenda kuwekwa | | Shehia | | | Mtaa/Barabara | | | | |

| *Kama ni Minara jaza hapa* | | | |
|---|---|---|---|
| Dhumuni la kuweka mnara | Pahala ulipowekwa | Wadi | |
| | | Shehia | |
| | | Mtaa | |

**4. TAMKO**

Mimi ______________________________ nathibitisha kwamba yote niliyoeleza hapo juu ni kweli kama nijuavyo, na kwamba nimekubaliana na masharti na taratibu zote za leseni kama zilivyo ainishwa katika fomu hii.

Tarehe uliyojaza fomu ____________ Sahihi ya muombaji

_______________

**5. KWA MATUMIZI YA OFISI TU**

| *Maoni kuhusiana na ombi lililoletwa* | | | |
|---|---|---|---|
| Afisa/Mkaguzi | Apewe/Asipewe | Tarehe | Muhuri na saini ya Afisa |
| Afisa wa kitengo cha Divisheni | | | |

| *Maoni ya Afisa Tathmini/Kitengo husika* | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kiwango anachostahiki kulipa | Faini | Jumla | Tarehe | Saini |
| | | | | |
| Imethibitishwa na Mkuu wa Idara ya Mipango, Utawala na Rasilimali Watu | | | | |

**6. MASHARTI YA MAOMBI NA UTHIBITISHO WA MUOMBAJI**

(i) Mteja au mfanyabiashara anatakiwa kufika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kufanya maombi ya leseni.

(ii) Muda wa hiari uliopangwa kukata leseni ya biashara kisheria ni kuanzia Januari hadi Machi. Na mara tu baada ya muda wa hiari kumalizika utalazimika kukata leseni pamoja adhabu ya faini ya 20% ya bei halisi ya leseni unayoomba.

(iii) Hakikisha kuwa unalipa ada ya usafi wa mazingira kwa wakati unaostahiki (kwa mwaka)

(iv) Hakikisha Fomu yako inaambatanishwa na vielelezo vinavyohusika kwa biashara zinazohusu ruhusa au uthibitisho wa Taasisi nyengine, biashara hizo ni kama maduka ya nyama, maduka ya dawa baridi, maduka ya Gesi, Kampuni, Vituo vya Afya, Skuli n.k. isipokuwa kwa vinavyomilikiwa na Serikali.

Scanned with CamScanner